

Jifunze kuhusu:

+ Wanyama na mimea ya kushangaza inayoishi karibu nasi na kwa nini tunaihitajia!




+ Jinsi mazingira asili yanasaidia kuhifadhi nyumba zetu, yanavyotulisha na kutuweka katika hali nzuri ya kiafya.



+ Jinsi ya kufaidika na maumbile bila ya kuyaharibu.

+ Kuchagua chakula cha bahari kwa busara ili kuhifadhi walobaki na viumbe vyengine.



+ Namna ya kujipatia riziki katika maisha na kulinda mazingira kwa faida ya baadae.



+ Kugeuza taka taka kuwa malighafi.

+ Namna tunavyofaidika tunaposafisha fukwe na jamii zetu.

+ Namna tunavyoweza kulinda mazingira yetu kwa faida ya baadae!

Chumbe Island Coral Park ni mradi wa hifadhi ya pwani ambao umejizolea sifa na zawadi nyingi kimataifa. Mradi huu unajiendesha wenyewe kupitia loji yake ya kimazingira ilipo katika kisiwa cha Chumbe. Ada ambayo wanalipa wageni hutumika kwa ufatlilaji na utafiti kwa matumbawe na pia hudhamini ziara za wanafunzi kwenda Chumbe kupata elimu ya mazingira kwa kila mwaka huenda wanafunzi wapato 500-600. Kisiwa kina nyumba za kulala wageni ambazo zimejengwa kwa usanifu, ubunifu na ujenzi ambao ni rafiki wa mazingira ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji ya mvua, nishati ya mwanga, maji ya moto yakanzwayo na jua, vyoo vya kutumia mbolea na maji machafu yanayochujwa kwa kutumia mimea.



Mazingira endelevu kwa Zanzibar

Coral Park



ISBN 978-9987-9467-2-3